# HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

## MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 13-14/05/2015

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma A. Kimisha | - | Diwani Kata ya Kisuke - Mwenyekiti |
| 2. | " Tabu R. Katoto | - | Diwani Kata ya Igunda-Makamu M/kiti |
| 3. | " Silvester Jilala | - | Diwani Kata ya Mapamba |
| 4. | " Makashi Emmanuel | - | Diwani Kata ya Sabasabini |
| 5. | " Mohamed A. Mwarabu | - | Diwani Kata ya Chona |
| 6. | " Sospeter N. Bunende | - | Diwani Kata ya Idahina |
| 7. | " Sayi S.Gamaya | - | Diwani Kata ya Ukune |
| 8. | " Joseph Masaluta | - | Diwani Kata ya Bulungwa |
| 9. | " Emmanuel Nding'wa | - | Diwani Kata ya Kinamapula |
| 10. | " Kulwa D.Shoto | - | Diwani Kata ya Bukomela |
| 11. | " Paul Magazi | - | Diwani Kata ya Uyogo |
| 12. | " Benedicto Mabuga | - | Diwani Kata ya Mpunze |
| 13. | " Pili E. Sonje | - | Diwani Kata ya Ushetu |
| 14. | " Pastory Nyororo | - | Diwani Kata ya Igwamanoni |
| 15. | " Paschal Mayengo | - | Diwani Kata ya Ulowa |
| 16. | " Doa Limbu | - | Diwani Kata ya Nyankende |
| 17. | " Kulwa Nyiriga | - | Diwani Kata ya Ulewe |
| 18. | " Damas J. Njige | - | Diwani Kata ya Chambo |
| 19. | " Hamis M. Mbogora | - | Diwani Kata ya Ubagwe |
| 20. | " Mary Lundalila | - | Diwani Viti Maalum |
| 21. | " Esther Imambo | - | Diwani Viti Maalum |
| 22. | " Eva P. Mkonya | - | Diwani Viti Maalum |
| 23. | Ndg.Isabela Chilumba | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu |

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

Mhe. James D. Lembeli - Mbunge Jimbo la Kahama –bila taarifa

WATAALAM WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Ndg. | Andrew Chikwanda | - | Afisa Mipango (W) |
| 2. " | Pastory Kayaga | - | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 3. " | Christina Akyoo | - | Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 4. " | Silvanus A. Bonda | - | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 5. Dr. | John Duttu | - | Kaimu Mganga Mkuu (W) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. Ndg. | Saulo E. Mkama | - | Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W |
| 7. “ | Gasati Silla | - | Kaimu Afisa Biashara (W) |
| 8. “ | Gervas Magogozwa | - | Afisa Utamaduni (W) |
| 9. “ | Marco Mwairwa | - | Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 10. “ | Deus Kakulima | - | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 11. Eng. | Charles Pambe | - | Kaimu Mhandisi wa Maji (W) |
| 12. Ndg. | Godson Kinkande | - | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |
| 13. “ | Onesmo Benjamin | - | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 14. “ | Melkiad P. Gaka | - | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 15. “ | Anna Ngongi | - | Afisa Kilimo na Ushirika (W) |
| 16. “ | Deogratias Rugangila | - | Afisa Ushirika (W) |
| 17. “ | Neuster James | - | Mwanasheria (W) |
| 18. “ | Benedicto Anthony | - | Mhasibu Mapato |
| 19. “ | Morgan Mwita | - | Mratibu wa kudhibiti UKIMWI |
| 20. “ | Jackson Wanyancha | - | Kaimu Afisa TEHAMA (W) |
| 21. “ | Valentina C. Majembe | - | Afisa Utumishi - TSD |
| 22. “ | Willibard Samamba | - | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |
| 23. “ | Magambo Makori | - | Mhasibu Matumizi |
| 24. “ | Juma R. Ngogo | - | Afisa Mipango Miji |
| 25. “ | Denis J. Pius | - | Mratibu wa TASAF |
| 26. “ | Victor Mhapa | - | Afisa Tawala H/W |
| 27. “ | Phillipo Karol | - | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 28. “ | Elinight Mmari | - | Kaimu Afisa Ugavi (W) |
| 29. “ | Yasini Said | - | Afisa Tawala (W) Kahama |
| 30. “ | Kawishe Lucas | - | Afisa Ufugaji Nyuki (W) |
| 31. “ | Emmanuel Kabelwa | - | Katibu wa Afya |
| 32. “ | Lucy Kihiyo | - | Afisa Ustawi wa Jamii |
| 33. Dr. | Idrisa Kabanda | - | Mganga |
| 34. Dr. | Nicodemus Senguo | - | Mganga |
| 35. Ndg. | Tumshukuru C. Mudui | - | Afisa Tarafa - Dakama |
| 36. “ | Salakana J. Peter | - | Afisa Tarafa - Mweli |

WAGENI WAALIKWA WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Insp | D.M. Misana | - | Mkuu wa Magereza (W) |
| 2. Ndg. | Mkama R.V. | - | Afisa TAKUKURU |
| 3. “ | Paschal John | - | Kny. Mkuu wa Polisi (W) |
| 4. “ | Paulo U | - | Afisa Uhamiaji |
| 5. “ | John Joel | - | Mwenyekiti CHADEMA - Ushetu |
| 6. “ | Mrisho Masoud | - | Mshauri wa Mgambo (W)- Kahama |
| 7. “ | Maliselina Komba | - | Kaimu Afisa Usalama wa Taifa (W) |

8. Ndg. Patrick Mabula - Mwandishi wa Habari - Majira
9. " Salvatory Kelvin - Mwandishi wa Hahari - Kahama FM
10. " Greyson Kakulu - Mwandishi wa Habari - TBC
11. " Mustapha Kapalata - Mwandishi wa Habari - Star TV
12. " Frank Mshana - Mwandishi wa Habari - ITV

SEKRETARIETI

1. Ndg. Chamo Mashauri - Mwandishi wa vikao
2. " Ashura Hoja - Mwandishi wa vikao
3. " Christina Ntelya - Mwandishi wa vikao

MUHT. NA. BM/48/2014/2015 – KUFUNGUA MKUTANO

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwakaribisha wajumbe, wataalam na wageni wote walioshiriki mkutano huo. Alieleza kuwa mkutano huo wa Baraza la madiwani ulikuwa umepangwa kufanyika tarehe 12-13/05/2015 lakini kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiutendaji hususani kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC), ililazimika kuahirishwa Baraza kwa siku moja.

Pia alieleza kuwa kutokana na kufanyika kikao cha wadau wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kujadili Sheria Ndogo za mfuko huo za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, imesababisha kuchelewa kuanza kwa mkutano wa siku hiyo.

Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha mwenyekiti kufungua mkutano.

Mwenyekiti aliwakaribisha wote walioshiriki mkutano na kueleza kuwa huo ni mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kujadili taarifa za robo ya tatu (Januari - Machi) 2014/2015 pamoja na masuala mbalimbali ya Halmashauri.

Mwenyekiti alifungua mkutano saa 06:26 mchana.

MUHT. NA. BM/49/2014/2015 – KURIDHIA AGENDA ZA MKUTANO

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha agenda 16 za mkutano huo, ambazo agenda 15 taarifa zake zilikuwa kwenye kablasha la mkutano na agenda kuhusu "Mapendekezo ya kuanzisha jimbo jipya la uchaguzi (jimbo la Ushetu) wilayani Kahama" iliwasilishwa kikaoni. Agenda hizo ni:-

Tarehe 13/05/2015

1. Kufungua mkutano
2. Kuridhia agenda za mkutano

3. Kusoma na kuthibitisha mihtasari ya mkutano wa
   Tarehe 27 – 28/01/2015 – mkutano maalum wa bajeti ya 2015/2016
   Tarehe 12 – 13/02/2015 – mkutano wa kawaida
4. Yatokanayo na muhtasari wa mkutano wa tarehe 12 – 13/02/2015
5. Taarifa ya mapato na matumizi mwezi Machi, 2015
6. Taarifa ya utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais kuhusu ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara kwa kila Shule ya Sekondari.
7. Mpango wa uendelezaji wa misitu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu
8. Taarifa za utekelezaji wa miradi ngazi ya kata
9. Maombi ya kukopa fedha Tshs. 300,000,00.00 kutoka akaunti ya maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa tipa na “low loader”
10. Mapendekezo ya kuanzisha jimbo jipya la uchaguzi (jimbo la Ushetu) wilayani Kahama
11. Mapendekezo ya eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kuwa Wilaya

Tarehe 14/05/2015

12. Maswali ya papo kwa papo
13. Maombi ya kibali cha kuajiri kwa mkataba madereva wawili (operators) wa mitambo.
14. Taarifa za Kamati za kudumu za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri na Bodi ya zabuni katika kipindi cha robo ya tatu (Januari – Machi, 2015)
    - Kamati ya kudhibiti UKIMWI
    - Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    - Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    - Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango
    - Bodi ya zabuni

15. Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kutembelea miradi ya maendeleo ya Halmashauri robo ya tatu (Januari – Machi, 2015) tarehe 28 – 30/04/2015
16. Kufunga kikao

Wajumbe waliridhia kujadili agenda zote 16 kama zilivyowasilishwa na Katibu.

MUHT. NA. BM/50/2014/2015 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHUTASARI

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari mmoja baada ya mwingine ukurasa kwa ukurasa. Wajumbe walibainisha masahihisho yafuatayo:-

i) Muhtasari wa Mkutano maalum bajeti ya 2015/2016 tarehe 27-28/01/2015

Uk. 1 - jina Mhe. Paul Magazi liandikwe Diwani kata ya Uyogo badala ya kata ya Ulowa

- wajumbe ambao hawakuhudhuria watajwe ni kwa taarifa au bila taarifa

ii) Muhtasari wa Mkutano wa kawaida tarehe 12-13/02/2015

Uk. 15 harambee ya ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha afya Ukune ilifanyika tarehe 31/08/2014 siyo mwaka 2007

Baada ya masahihisho hayo, wajumbe walisema kuwa ni mihutasari sahihi hivyo Katibu na Mwenyekiti walitia saini kwa ajili ya kumbukumbu za Halmashauri.

MUHT. NA. BM/51/2014/2015 - YATOKANAYO NA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 12 – 13/02/2015

Maelezo ya utekelezaji yalitolewa kama ifuatavyo:-

Kutoka Muhtasari Na. BM/37/2014/2015 Kuhusu ziara ya China iliyofanywa na Mkurugenzi Mtendaji (W) na Mwenyekiti wa Halmashauri.

Taarifa ya ziara hiyo iliwasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) na wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Mohamed A. Mwarabu alitaka kujua kiasi cha gharama za ziara hiyo na kama zimetolewa na mfadhili au Halmashauri

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema kuwa gharama ya ziara hiyo ilitolewa na Halmashauri kupitia ruzuku ya Serikali (Capacity Building Grant) pamoja na ufadhili wa ALAT. Alieleza kuwa ameandaa taarifa ya ziara kama Baraza lilivyoomba ikiwa ni maeneo waliyotembelea, vikao walivyofanya na masuala kadha waliyojifunza. Kama wajumbe wanahitaji kujua gharama zilizotumika, ataziwasilisha kikao kijacho.

Kutoka Muhtasari Na. BM/45/2014/2015

i) kuhusu wanafunzi wa kidato cha V & VI wanaolipiwa ada na Halmashauri

Ilielezwa kuwa kwa sasa Halmashauri inatambua orodha ya wanafunzi wanaolipiwa ada walio kidato cha I hadi IV

Mhe. Mohamed A. Mwarabu alisema kuwa wanafunzi wa kidato cha V & VI wasio na uwezo wagharamiwe na Halmashauri katika ada na hela ya mitihani ya Taifa.

Mhe. Sospeter Bunende na Mhe. Paul Magazi walichangia kuwa wanafunzi wote waliogharamiwa ada na Halmashauri katika kiwango cha kidato cha I hadi IV, Halmashauri iendelee kuwalipia ada na fedha za mitihani ya Taifa mara wakichaguliwa kuingia kidato cha V & VI katika shule za Serikali.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema kuwa kama Baraza la Madiwani litaridhia, yuko tayari kutekeleza.

Mwenyekiti alihitimisha kuwa Baraza la Madiwani limeridhia wanafunzi wote wanaogharamiwa ada na Halmashauri katika kiwango cha kidato cha I hadi IV, Halmashauri itaendelea kuwalipia ada na fedha za mitihani ya Taifa mara wakichaguliwa kuingia kidato cha V & VI katika shule za Serikali.

ii) Kuhusu taarifa kamili ya ujenzi wa maabara za shule za sekondari
Taarifa hiyo iliandaliwa na kuwasilishwa mkuatanoni kama ajenda kamili yaani agenda namba BM/53/2014/2015

MUHT. NA. BM/52/2014/2015 - TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI MACHI, 2015

Kaimu Hazina (W) aliwasilisha taarifa ya Mapato na matumizi mwezi Machi, 2015 kama ifuatavyo:-

| Na | Mapato | Makisio kwa mwaka | Mwezi Machi 2015 | Julai – Machi 2014/2015 | Asili mia |
|---|---|---|---|---|---|
| a) | MAPATO YA NDANI | 2,025,000,000.00 | 37,848,382.2 | 2,043,756,339.42 | 101 |
| | Ruzuku, mishahara na miradi ya maendeleo | 18,240,413,194.00 | 1,400,834,237.25 | 11,376,035,760.53 | 62 |
| b) | MATUMIZI | | | | |
| | Fedha za Ndani | 951,750,000.00 | 61,521,650.97 | 893,000,183.44 | 93.83 |
| | Ruzuku | 12,824,905,367.19 | 739,326,533.33 | 9,493,567,119.78 | 74.02 |
| | Miradi ya Maendeleo (Fedha za Ndani) | 1,073,250,000.00 | 101,915,700.00 | 419,119,000.02 | 39 |
| | Miradi ya Maendeleo (Fedha za Ruzuku) | 6,198,307,934.00 | 267,747,017.00 | 1,492,006,477.48 | 24.07 |

Alieleza kuwa mapato ya mishahara yanajumuisha watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na Mji wa Kahama

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Mhe. Joseph Masaluta alishauri kuwa mara tu baada ya mitambo ya kutengeneza barabara kuzinduliwa, kazi ya kwanza iwe ni kutengeneza barabara ya Karo – Bulungwa ambayo ni mbovu kwani pia hutumika katika usafirishaji wa mazao ya kilimo. Hoja hii iliungwa mkono na Mhe. Emanuel Makashi na Mhe. Sospeter Bunende.

Wajumbe wengine waliojadili, walipongeza kuongezeka kwa mapato ya ndani ambayo hadi Machi, 2015 yamefikia asilimia 101. Pia walipongeza Halmashauri kutekeleza azma ya ununuzi wa mitambo ya kutengeneza barabara kama ilivyo katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

## MUHT. NA. BM/53/2014/2015 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA AGIZO LA MHE. RAIS KUHUSU UJENZI WA VYUMBA VITATU VYA MAABARA KWA KILA SHULE YA SEKONDARI.

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa hiyo na kusema kuwa ujenzi wa vyumba vya maabara ulianza mwezi Oktoba, 2015 kwa shule 15 za sekondari mara tu baada ya kupokea agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vyumba vinavyohitajika ni 45 ikiwa ni vyumba 3 kwa kila shule. Ujenzi huu ulianza kwa kuhamasisha wananchi kuchangia fedha kwa makubaliano ya michango katika kaya na kwa wale waliokosa uwezo walichangia nguvu kazi. Halmashauri ilichangia gharama kadhaa ili kuharakisha ujenzi wa maboma ikiwa ni kulipia gharama za ufundi, kuwapatia saruji , usafiri kwa ajili ya kubebea mchanga, mawe na kokoto.

Katika bajeti ya 2014/2015, Halmashauri ilibadili matumizi ya Tshs. 507,000,000.00 ili ziasaidie katika ujenzi wa maabara kwa kuangalia miradi iliyokuwa ikitekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani na fedha za ruzuku toka serikali kuu. Mpaka sasa changamoto ipo kwa fedha za miradi ya ruzuku ya maendeleo ambazo hazijapatikana zote,hivyo kiasi kilichopatikana ni fedha toka mapato ya ndani tu.

Utaratibu uliotumika ulikuwa ni wa kazi kusimamiwa na timu ya wataalamu wa Halmashauri ikiongozwa na Wahandisi wa Ujenzi na Wataalamu wa Ugavi wa Halmashauri kwa kununua bidhaa wenyewe na kusimamia ujenzi wenyewe (force account).

Alisema kuwa katika kipindi cha Oktoba 2014 hadi Aprili 2015 Halmashauri imetekeleza yafuatayo katika ujenzi wa maabara:-

(i) Kununua mabati yote yaliyotumika kupaulia vyumba vya maabara, geji 28 toka kiwanda cha ALAF – Dar es Salaam kwa gharama ya Tsh 98,000,000.00

(ii) Kununua mbao zote zilizotumika kupaulia maabara zote kwa Tsh, 56,000,000.00

(iii) Kununua vigae (tiles) toka Dar es salaam kwa Tsh 46,000,000.00

(iv) Kununua madirisha ya “aluminium na grills” kwa Tsh 46,590,000.00

(v) Kununua mifuko ya saruji 2416 yenye thamani ya Tsh 40,347,200.00

(vi) Kutengeneza milango kwa vyumba vyote 26 kwa Tsh 15,600,000.00

(vi) Kununua mabomba ya maji, sinki, vifaa vya mifumo ya gas, meza na stuli za maabara kwa Tsh 88,046,900.00

Halmashauri ilipata michango ya jumla ya Tsh 10,000,000.00 toka LAPF na Pan African Ltd.

Mkurugenzi aliendelea kueleza kuwa jumla ya gharama za ujenzi wa vyumba 45 vya maabara mpaka sasa ni Tsh.1, 132,845,458.10 michango ya wananchi Tsh. 179,685,100.0 na mchango wa Halmashauri Tsh. 953,160,358.1 Gharama za ujenzi wa maabara katika kila shule na hatua zilizofikiwa katika ujenzi ziliambatanishwa.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Mohamed A. Mwarabu alieleza kuwa mtindo wa manunuzi wa “force account” uliotumika katika ujenzi wa maabara umeonekana kuwa na tija zaidi kwani majengo ya maabara yana ubora kutokana na usimamizi thabiti wa wataalam waliokabidhiwa. Pia mtindo huo wa manunuzi umeipunguzia gharama kubwa Halmashauri tofauti na gharama za kutangaza zabuni. Aliomba Halmashauri isaidie katika kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mwalimu shule ya sekondari Chona.

Mhe. Sospeter Bunende aliunga mkono maoni ya Mhe. Mwarabu kuhusu mtindo wa manunuzi wa “force account”. Alitaka kujua kama Halmashauri itakamilisha ujenzi wa maabara kwa wakati ili kutekeleza lengo la mkoa.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa kwa sasa Halmashauri haina fedha ya kutekeleza miradi mingine kwani fedha zinazopatikana zimeelekezwa kwenye ujenzi wa maabara. Pia alisema kuwa Halmashauri inakusudia kukamilisha ujenzi wa maabara kwa wakati ili kukidhi malengo (muda) ya mkoa na Taifa.

Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kutambua na kuthamini kazi kubwa ya ujenzi wa maabara jinsi inavyotekelezwa. Alishauri kuwa kasi iongezwe zaidi kwenye kata ambazo ujenzi wa maabara zake uko nyuma.

MUHT. NA. BM/54/2014/2015 - MPANGO WA UENDELEZAJI WA MISITU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

Afisa Ardhi na Maliasili (W) aliwasilisha taarifa hiyo alisema kuwa katika mpango kuna shughuli mbalimbali zitakazotekelezwa ili kufikia uhifadhi, uendelezaji na utunzaji wa misitu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Kazi zilizoainishwa katika mpango huo ni:-

1. Utambuzi wa aina ya miti iliyomo misituni na kujua jumla ya ujazo wake kwa kila aina.
2. Udhibiti uchomaji moto kiholela katika misitu.
3. Maelekezo sahihi ya uangushaji wa miti kwa ajili ya mbao, mkaa, kuni, nguzo, fito na mazao mengine ya misitu.
4. Udhibiti wa kilimo na ufugaji mifugo katika misitu.
5. Utambuzi na upimaji wa mipaka ya misitu, kupima na kutangaza misitu mipya hasa ya vijiji.
6. Uendelezaji wa misitu hii kwa kuwezesha uoto wa asili, urejeshaji na upandaji miti ya asili na isiyo ya asili.
7. Uanzishaji wa bustani za miche ya miti.
8. Kuwezesha hifadhi ya ardhi na udongo.
9. Kuwezesha upatikanaji zaidi wa watumishi wa kitengo cha misitu na nyuki.
10. Uelimishaji jamii juu ya kuhifadhi na kuendeleza misitu na manufaa yatokanayo na shughuli hizo.
11. Kuelimisha wafugaji nyuki ili kuweza kupata mavuno mengi zaidi na yaliyo bora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.
12. Gharama zitakazohusika katika kutekeleza shughuli zote zilizomo katika mpango
13. Ufuatiliaji na uperembaji wa shughuli zitakazo tekelezwa katika mpango.

Baada ya kuwasilisha, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Emanuel Nding`wa alieleza kuwa anakubaliana na mpango wa uendelezaji wa hifadhi ya misitu. Alisema kuwa inatakiwa wajumbe wafanye ziara ya kukagua misitu na mipaka yake kisha wajadili mpango wakiwa na picha halisi ya misitu wanayoijadili.
Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa wajumbe wote wanaifahamu misitu iliyo ndani ya Halmashauri yetu hivyo hakuna haja ya kufanya ziara. Hata hivyo, katika bajeti ya mwaka 2014/2015, hakuna bajeti kwa ajili ya ziara ya kutembelea misitu na kwamba fedha nyingi za mapato ya ndani na ruzuku ya serikali imeelekezwa katika ujenzi wa maabara za shule za sekondari.

Mhe. Paul Magazi aliunga mkono mapendekezo ya uendelezaji wa misitu katika Halmashauri yetu. Alitaka kujua utatuzi wa mgogoro wa msitu wa Usumbwa umefikia wapi

Afisa Ardhi na Maliasili (W) alieleza kuwa mgogoro huo unatatuliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Urambo. Kazi 13 zilizotajwa kwenye mpango zitasaidia sana katika uendelezaji wa misitu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Mwenyekiti alisema kuwa Baraza la Madiwani limeridhia mpango wa uendelezaji wa misitu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu

MUHT. NA. BM/55/2014/2015 - TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI NGAZI YA KATA
Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kata za Idahina, Ulowa, Sabasabini na Ubagwe ziliwasilishwa na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

Mhe. Emanuel Makashi aliomba Serikali kuanzisha mfuko wa kuchochea maendeleo ya kata ili madiwani waweze kusaidia katika kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zao.

Mhe. Mohamed A. Mwarabu alisema kuwa taarifa zinazowasilishwa ziwe zinafanyiwa kazi, kwani alishaomba Mhandisi wa Ujenzi (W) aende kukagua miradi ya ujenzi katani kwake mathalani kijiji cha Itebele ili hatua zaidi za ujenzi ziweze kuendelea lakini hakuna utekelezaji uliofanyika. Pia aliomba Halmashauri kusaidia katika kukamilisha ujenzi wa miradi kama inavyowasilishwa kwenye taarifa za kata.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa wataalam wa Idara ya Ujenzi watatembelea miaradi hiyo. Kuhusu Halmashauri kukamilisha miradi ya ujenzi, alieleza kuwa Halmashauri kwa sasa imejikita katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara kwa kila shule ya sekondari. Kuhusu mfuko wa kuchochea maendeleo ya kata, alisema kuwa ushauri huo ni mzuri lakini suala hilo ni la kitaifa.

MUHT. NA. BM/56/2014/2015 - MAOMBI YA KUKOPA FEDHA TSHS. 300,000,00.00 KUTOKA AKAUNTI YA MAENDELEO KWA AJILI YA UNUNUZI WA TIPA NA "LOW LOADER"

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa hiyo. Alieleza kuwa ili kukamilisha matumizi ya mitambo hiyo, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu iliidhinishiwa jumla ya Tshs. 350,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa lori moja la kubebea mitambo na gari dogo aina ya landcruiser Hardtop lakini hadi hivi sasa fedha hiyo haijaletwa.

Alisema kutokana na hali halisi ya ununuzi wa mitambo ya barabara ambayo ilifanywa na kampuni ya Pan African na kuikabidhi Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu tarehe 28/04/2015 ikiwa ni pamoja na shindilia moja (vibrator roller) na grader moja na vyote hivyo vipo katika eneo la ofisi za Halmashauri.

Ili mitambo hiyo iweze kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Wilaya, inahitajika kuwa na lori la kubebea (low loader) pamoja na tipa kwa ajili ya kubeba vifusi vya barabara.

Aidha, alieleza kuwa kwa kuwa fedha iliyokasimiwa imechelewa kuja toka Hazina, aliomba mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kuidhinisha Tshs. 300,000,000.00 kama mkopo toka akaunti ya maendeleo kwa fedha zilizokusudiwa kwa ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ili zitumike kununua lori la kubebea mitambo ambayo ni Tshs. 200,000,000.00 na lori moja (tipper) la tani 8 ambayo ni Tshs. 100,000,000.00. Fedha hizo zitarejeshwa mara fedha toka Serikalini itakapoletwa na pia kulipwa kupitia mapato ya ndani. Mabadiliko ya gharama halisi yanaweza kutokea kutokana na mabadiliko ya thamani ya dola za kimarekani.

Baada ya maombi hayo kuwasilishwa, wajumbe wote waliafiki Tshs. 300,000,000.00 zikopwe kutoka akaunti ya maendeleo na zitumike kununua "low loader" moja na "tipper" moja la tani 8.

MUHT. NA. BM/57/2014/2015 - MAPENDEKEZO YA KUANZISHA JIMBO JIPYA LA UCHAGUZI (JIMBO LA USHETU) KATIKA WILAYA YA KAHAMA

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya agenda hiyo. Alieleza kuwa kutokana na barua ya Mkurugenzi wa Uchaguzi kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi yenye Kumb. Na. AB.42/74/02 ya tarehe 10 Mei, 2015 imeelekeza vigezo na utaratibu utakaotumika kugawa majimbo, kurekebisha mipaka au kubadili majina, kuwa:-

- Maombi yatawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika ambapo yatajadiliwa katika vikao rasmi. Vikao hivyo vitashirikisha wadau mbalimbali
- Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha maombi/mapendekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa
- Katibu Tawala wa Mkoa atawasilisha maombi/mapendekezo katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ili kupata maoni zaidi
- Katibu Tawala wa Mkoa atawasilisha mapendekezo Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa barua huyo, vigezo vitakavyotumika kugawa majimbo ni:-

i) Mgawanyo wa wastani wa idadi ya watu (population quota)
ii) Idadi ya watu
iii) Upatikanaji wa mawasiliano
iv) Hali ya kijiografia
v) Hali ya uchumi
vi) Ukubwa wa eneo la jimbo husika
vii) Mipaka ya kiutawala
viii) Jimbo moja lisiwe ndani ya Wilaya/Halmashauri mbili
ix) Kata moja isiwe ndani ya majimbo mawili
x) Mpangilio wa maeneo ya makazi ya watu yaliyopo (existing pattern of human settlement)
xi) Mazingira ya Muungano
xii) Uwezo wa ukumbi wa bunge
xiii) Viti Maalum vya Wanawake

Alieleza kuwa kutokana na kuanzishwa kwa Halmashauri tatu (3) wilayani Kahama yenye majimbo mawili (2) tu ya uchaguzi yaani Jimbo la Kahama na Jimbo la Msalala, hali hiyo imesababisha mwingiliano katika mgawanyo wa kiutawala. Mathalani Jimbo la Kahama lenye Kata 34, Kata 20 zipo Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na Kata 14 zipo Halmashauri ya Mji wa Kahama na kwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, Tarafa Isagehe (Kata zake) imeingiliana na Halmashauri ya Mji wa Kahama ambalo ni Jimbo jingine yaani Jimbo la Kahama.

Alieleza kuwa inahitajika kuazishwa Jimbo la tatu (3) katika Wilaya ya Kahama yaani Jimbo la Ushetu ili kutatua mwingiliano huo. Alisema kuwa eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu lenye $km^2$ 5311.0 na wakazi 303,386 liwe Jimbo la uchaguzi na liitwe Jimbo la Ushetu. Halmashauri hii ina eneo kubwa

zaidi na idadi kubwa ya watu. Jimbo hili la Ushetu litakuwa na Kata zote 20 za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ambazo ni Mapamba, Bukomela, Igunda, Mpunze, Kisuke, Sabasabini, Ukune, Kinamapula, Nyankende, Chambo, Igwamanoni, Uyogo, Ubagwe, Ushetu, Ulewe, Chona, Ulowa, Idahina na Bulungwa na Nyamilangano.

Baada ya kuwasilisha wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Pili Sonje alieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ina idadi kubwa ya watu inayokidhi kuwa jimbo. Pia kuna mwingiliano wa mipaka ya kutawala hali inayosababisha utendaji kuwa mgumu. Alisema kuwa ni muda muafaka kuhakikisha linaanzishwa Jimbo jipya la Uchaguzi la Ushetu.

Mhe. Kulwa Shoto aliunga mkono mapendekezo ya kuanzisha Jimbo jipya la Uchaguzi la Ushetu. Alisema kuwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, itakuwa vigumu kusimamia uchaguzi huo hususani Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi kwani jimbo la Kahama lina Halmashauri mbili yaani Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na Halmashauri ya Mji wa Kahama. Aliunga mkono mapenekezo ya kuanzisha Jimbo jipya la Uchaguzi la Ushetu.

Mhe. Damas J. Njige alisema kuwa mapendekezo ya kuanzishwa Jimbo (jipya) la Uchaguzi la Ushetu walishayaafiki wakati walipoalikwa kuhudhuria kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) kilichofanyika tarehe 19/09/20114. Alisema kuwa suala la eneo la Ushetu kuwa jimbo walilitamani sana siku nyingi.

Mwenyekiti alisema kuwa wajumbe kwa pamoja wameafiki mapendekezo ya kuanzisha Jimbo jipya la Uchaguzi la Ushetu. Aliagiza kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) ahakikishe anawasilisha mapendekezo hayo kwa mamlaka husika mapema iwezekanavyo na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wake.

MUHT. NA. BM/58/2014/2015 MAPENDEKEZO YA ENEO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU KUWA WILAYA

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa hiyo, alieleza kuwa kupitia kikao cha kawaida cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango tarehe 30/04/2015, wajumbe waliridhia eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kuwa Wilaya kamili, waliomba agenda hiyo iwasilishwe kwenye Baraza tukufu kwa hatua zaidi za maridhianao.

Mkurugenzi alieleza kuwa:-

1. Eneo la Ushetu lina Halmashauri moja ya Wilaya ambayo imeanzishwa rasmi tarehe 23/11/2012 kupitia gazeti la serikali namba 362/2012. Kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ina eneo la kilomita za mraba 5,311 sawa na asilimia 56.1 ya eneo la wilaya ya Kahama

2. Kiutawala, Halmashauri ya wilaya ya Ushetu ina jimbo 1 la uchaguzi la Kahama, Tarafa 2, Kata 20, vijiji 112, na vitongoji 554. Kwa upande wa watumishi, Halmashauri ina watumishi 1,810

3. Idadi ya wakazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ni 273,023, (kwa mujibu wa sensa ya 2012 na kiwango cha ongezeko la watu ni 3.7% kwa mwaka.

4. Hali ya Kiuchumi, eneo hili la Ushetu limejaaliwa kuwa na fursa kubwa katika kilimo cha mazao ya biashara na chakula. Kwa ujumla Ushetu inazalisha kwa kiasi kikubwa zao la mahindi, karanga, maharage na mpunga kwa wastani wa tani 673,958 kwa mwaka. Hivyo huifanya wilaya hii kuzalisha ziada kulinganisha na mahitaji yaliyopo.
5. Kwa upande wa mazao ya biashara, eneo la Ushetu linalima tumbaku, pamba na alizeti kwa wastani wa tani 47,647. Aidha katika mkoa wa Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inaongoza katika uzalishaji wa tumbaku na hivyo kuipatia Halmashauri ya wilaya mapato makubwa kwa wastani wa Tshs 1,046,000,000.00 kwa mwaka. Pia kuna misitu mikubwa ya asili na ya kupandwa yenye uwezo wa kuzalisha mbao, kuhifadhi mazingira, kuendeleza ufugaji wa nyuki, ng'ombe n.k. fursa hii ni chanzo kikubwa cha mapato kwa wilaya na Taifa. Sekta ya mifugo ina hudumia jumla ya ng'ombe 127,342, mbuzi 132,378, kondoo 24,136, nguruwe 804, mbwa 13,129 na kuku 480,207. Kuna majosho 10, malambo 6, vibanio 7, kituo cha kuhudumia mifugo 1.
6. Hali ya biashara katika eneo la Ushetu lina jumla ya wafanyabiashara wadogowadogo 1650. Uwekezaji na uanzishwaji wa viwanda katika eneo la Ushetu kutokana na fursa zilizopo inafaa kuanzisha viwanda vya mbao, useremala, viwanda vya vifaa vya kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Halmashauri imeanzisha mchakato wa kupima vituo vya kibiashara (trade centers) 8 ambavyo maeneo ya viwanda yatatengwa.

   Uchimbaji madini, Halmashuri ya wilaya ya Ushetu ina eneo moja la wachimbaji wa dhahabu wadogowadogo linalokadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 600 katika kata ya Idahina kijiji cha Mwabomba

7. Hali ya mawasiliano ni nzuri katika eneo la Ushetu kwa kuwa kuna makampuni mbalimbali za simu kama Tigo, TTCL, Vodacom, Zantel na Airtel. Kwa upande wa nishati ya umeme, bado sehemu kubwa ya wilaya ya Ushetu haina huduma ya umeme. Hata hivyo nguzo za umeme zinaendelea kusambazwa katika Kata za Mpunze, Sabasabini na Bulungwa ili kuwapatia wananchi umeme

8. Hali ya huduma za kijamii katika eneo hili la Ushetu ni nzuri kwani lina jumla ya shule za msingi 100 na shule 18 za sekondari zenye kidato cha I-IV, pia Halmashauri ya Wilaya ina mchakato wa kuanzisha (kufungua) kidato cha 5 katika shule ya sekondari Dakama mwaka 2015.

   Huduma ya Maji, Asilimia 47 ya wakazi wa vijiji hupata maji safi na salama kutoka katika visima vifupi, virefu, matanki ya kuvuna maji ya mvua, visima vya asili na malambo. Miradi mikubwa ya usambazaji wa maji ipo katika kata za Bulungwa, Nyamilangano na Ushetu.

   Idara ya Afya inatoa huduma za kinga na tiba katika vituo mbali mbali vya kutolea huduma, Jumla ya vituo vya kutolea huduma na tiba ni 22.

   Ukusanyaji mapato kwa vyanzo vya ndani kwa kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2015 Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu imeweza kukusanya kwa asilimia 101.

9. Idara ya polisi, Usalama wa Taifa, Mahakama ya Wilaya, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na nyinginezo zitaongezwa kutokana na uwepo wa Wilaya

   Mipaka ya wilaya itakuwa kama ilivyoainishwa na uwepo wa Halmashauri ya wilaya ambayo ipo katika tangazo la serikali kupitia gazeti namba 362/2012.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Sospeter Bunende alisema kuwa Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu lakini eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ni kubwa yaani kilomita za mraba 5,311 sawa na asilimia 56.1 ya eneo la wilaya ya Kahama. Alisema kuwa hii ni sifa kuu inayoshawishi kuomba eneo hilo kuwa Wilaya kamili. Alishauri

kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) na Mwenyekiti wa Halmashauri wafuatilie kwa karibu na ikibidi wamuone Waziri Mkuu kwa hatua zaidi za utekelezaji.

Mhe. Paschal Mayengo aliafiki suala la kuanzishwa kwa Wilaya ya Ushetu. Alisema kuwa mara tu baada ya kuanzisha Halmashauri ya wilaya ya Ushetu, mchakato wa kuanzisha Wilaya ungefuata mara moja.

Mhe. Kulwa Shoto alieleza kuwa eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu limekidhi vigezo vyote vya msingi kuweza kufanywa kuwa Wilaya. Alishauri mchakato uendelee kwa kuwasilisha vielelezo kwenye mamlaka husika.

Pia litaka kujua mchakato wa kuanzisha Jimbo la Uchaguzi la Ushetu umefikia wapi tangu kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) kuridhia suala hilo Oktoba 19, 2014.

Mkurugenzi Mtendaji (W) – Ushetu alifafanua kuwa tayari ameshawasilisha mapendekezo hayo Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa hatua zaidi.

Baada ya majadiliano, Mwenyekiti alisema kuwa wajumbe wameridhia uanzishaji wa Wilaya (mpya) ya Ushetu ambayo eneo la mipaka yake litakuwa ni eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Alieleza kuwa yuko tayari (itakapobidi) kufika Ofisi ya Waziri Mkuu kufuatilia suala hilo.

## Kuahirisha mkutano

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa kabla ya kuanza mkutano wa Baraza la Madiwani tarehe 14/05/2015, kutakuwa na hafla fupi ya uzinduzi wa mitambo ya kutengeneza barabara ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu itakayozinduliwa na Mkuu wa Wialaya ya Kahama Ndg. Benson Mpesya. Mara tu baada ya zoezi la uzinduzi, mkutano utaendelea. Aliwaalika wajumbe wote kushiriki uzinduzi huo. Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha Mwenyekiti kuahirisha mkutano

Mwenyekiti aliahirisha mkutano saa 10:26 jioni na kueleza kuwa mkutano utaendelea siku inayofuata tarehe 14/05/2015.

## Mwendelezo wa mkutano

Mwenyekiti aliendeleza mkutano tarehe 14/04/2015 saa 06:02 mchana

MUHT. NA. BM/59/2014/2015 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO

Mwenyekiti alieleza kuwa hadi mkutano huo unaanza, alikuwa amepokea jina la Mhe. Emanuel Ndingwa kuwa angeuliza swali la papo kwa papo, lakini hadi wakati agenda hiyo imefikiwa, muuliza swali huyo hakuwepo ndani ya ukumbi wa mkutano hivyo aliruhusu agenda nyingine ziendelee.

MUHT. BM/60/2014/2015 - MAOMBI YA KIBALI CHA KUAJIRI KWA MKATABA MADEREVA WAWILI (OPERATORS) WA MITAMBO.

Kaimu Afisa Utumishi (W) aliwasilisha maombi hayo na kueleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kupitia chanzo cha mapato ya ndani imefanikiwa kununua mitambo ya barabara yaani “motor grader na vibrating roller”. Aidha, mitambo hiyo tayari imewasili hapa Halmahauri na kukabidhiwa kwenye mamlaka husika.

Alieleza kuwa bajeti ya madereva wa mitambo ipo kwenye mpango wa mwaka wa fedha 2015/2016 hivyo anaomba kibali ili kuweza kuajiri madereva (operators) wawili kwa ajili ya kuendesha mitambo hiyo. Madereva hawa wataingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa kipindi cha miezi mitatu (3) na mkataba utakuwa endelevu hadi pale Halmashauri itakapoajiri madereva wa kudumu au Halmashauri itakapoamua (kwa muda wowote) kuwaachisha kazi.

Baada ya maombi hayo kuwasilishwa, wajumbe wote waliunga mkono maombi hayo ya ajira.

MUHT. NA. BM/61/2014/2015 - TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI NA BODI YA ZABUNI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI, 2015)

A: KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati Mhe. Tabu Katoto aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo iliyotokana na vikao vifuatavyo:-

- Kikao maalum cha bajeti cha tarehe 08/01/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 23/04/2015
- Kikao cha kawaida cha tarehe 23/01/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 23/04/2015
- Kikao cha Kawaida cha tarehe 23/04/2015 ambacho muhtasari wake utathibitishwa kikao kijacho

Muhtasari Na. UK/02/2014/2015
Kamati ilipitia, kujadili kisha kuridhia mapendekezo ya mpango wa bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa ajili ya shughuli za kudhibiti VVU/UKIMWI ikiwa ni kiasi cha shilingi 72,460,934.00 ambapo Tshs.5,000,000.00 zitatokana na mapato ya ndani na Tshs.67,460,934.00 zitatoka NMSF.
Makisio ya bajeti za wadau wa mwitikio dhidi ya UKIMWI wanaoshirikiana na Halmashauri ni Tshs. 273, 000,000.00

Muhtasari Na. UK/16/2014/2015 - Taarifa ya utekelezaji shughuli za kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Desemba) 2014 iliwasilishwa na kujadiliwa ambapo kamati ilitoa mapendekezo ya namna ya upatikanaji wa wawakilishi wa jumuia na (au) asasi mbalimbali kama ilivyo katika mwongozo.

Tayari utekelezaji umeshafanyika na kamati yenye muundo mpya imeanza kufanya kazi za kudhibiti VVU/UKIMWI tangu April, 2015.

<u>Taarifa ya utekelezaji shughuli za mwitikio wa kudhibiti VVU/UKIMWI kwa kipindi cha robo ya tatu (Januari – Machi) 2015</u>

Ilielezwa kuwa huduma za matibabu na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI
Kwa kipindi cha Januari 2015 hadi Machi 2015, asasi ya REICHET na SHIVYAWATA ndizo zilifanikiwa kutekeleza majukumu yao

Halmashauri imepokea fedha za NMSF Tshs 73,991,000 mwishoni mwa robo ya tatu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kudhibiti UKIMWI katika maeneo manne ya kipaumbele.

Katika kipindi cha utekelezaji cha robo ya 3, Januari 2015 hadi Machi 2015, Halmashauri imefanikiwa kutumia Tshs 1,837,500 kati ya Tshs 20,940,128 zilizopangwa kutumika, sawa na asilimia 8.76 ya matumizi katika kutekeleza afua mbalimbali za mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI kupitia vyanzo 2 vya fedha (NMSF na Mapato ya ndani).

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo.

B: KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA
Mwenyekiti wa kamati Mhe. Paschal Mayengo aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo iliyotokana na vikao vifuatavyo:-

- Kikao maalum cha bajeti cha tarehe 14/01/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 22/04/2015

- Kikao cha kawaida cha tarehe 30/01/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 22/04/2015

Taarifa za utekelezaji wa shughuli za halmashauri robo ya pili, Oktoba - Desemba 2014 za Idara za Mipango na Takwimu, Kilimo na Ushirika, Mifugo na Uvuvi, Ardhi na Maliasili, Ujenzi na Idara ya Usafi na Mazingira ziliwasilishwa

Katika kipindi cha robo ya tatu, Januari – Machi 2015 Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ilipitia na kujadili taarifa za utekelezaji 2015 ambazo muhtasari wake bado haujathibitishwa.

1. Taarifa za Idara zifuatazo ziliwasilishwa na kujadiliwa:-
   - Idara ya Mipango na Takwimu
   - Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
   - Idara ya Mifugo na Uvuvi
   - Idara ya Usafi na Mazingira
   - Idara ya Ujenzi
   - Idara ya Ardhi na Maliasili
   - Kitengo cha Ufugaji Nyuki
   - TASAF III

2. Mapendekezo ya kutangaza Miji 13 ya biashara (trading centres) kuwa maeneo ya Mipango Miji (planning area) ambapo miji ifuatayo iliridhiwa kuwa maeneo ya Mipango Miji;- Mbika, Kangeme, Nyamilangano, Mseki, Chambo, Mwadui, Nyankende, Uyogo, Mpunze, Iboja, Bugomba B, Iramba na Nyamtengela.

3. Taarifa ya mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu (CBPP) na ugonjwa wa miguu na midomo (FMD) katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu iliwasilishwa na kujadiliwa ambapo wajumbe walikubaliana:-
   - Kuweka vizuizi vya ndani ili ugonjwa huo usienee zaidi
   - Kutoa chanjo kwa mifugo yote iliyomo katika maeneo hatarishi ambapo kila mfugaji atachangia shilingi 500/= kwa kila mfugo utakaochanjwa.
   - Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuona kama ugonjwa umekwisha.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-
Mhe. Mohamed A. Mwarabu alisema kuwa kuna utata kuhusu eneo la shamba la Nyamilangano kuwa la SHIRECU au la serikali ya kijiji. Alishauriwa kuwa suala hilo lifuatiliwe ili kumaliza utata uliopo.

Pia eneo la msitu wa Mpunze kuendelea kuvamiwa kwa shughuli za kiuchumi kinyume na sheria. Alishauri ufumbuzi utafutwe kwani limekuwa ni suala la muda mrefu.

Mwenyekiti alisema ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ifuatilie kutatua changamoto zilizotajwa.

Mhe. Sospeter Bunende alitaka kujua ni lini kitengo cha mifugo kitapeleka chanjo ya mifugo Kata ya Idahina kama walivyomwahidi Diwani huyo.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema suala la SHIRECU na msitu wa Mpunze litafanyiwa kazi. Kuhusu chanjo ya mifugo, alisema dawa tayari zimeshapatikana hivyo chanjo itaanza kutolewa hivi karibuni.

C: KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI

Mwenyekiti wa kamati Mhe. Pastory Nyororo aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo kutokana na kikao maalum cha bajeti cha Kamati ya Elimu, Afya na Maji kilichofanyika tarehe 15/01/2015 na kikao cha kawaida cha tarehe 29/01/2015.

Pia ilielezwa kuwa Halmashauri imetekeleza shughuli za:-

- Ujenzi wa maabara za sayansi 45 hadi kufikia mwezi Machi 2015 jumla ya vyumba vya maabara 19 vilikuwa vimekamilika na vyumba 26 viko katika hatua ya ukamilishaji. Gharama zilizotumika ni fedha toka Halmashauri ya Wilaya/Serikali kuu shilingi 888,706,757.90, michango ya wananchi pamoja na wadau wengine shilingi 177,217,700.00 na kuwa jumla ya fedha ni shilingi 1,065,924,457.90.
- Ukamilishaji wa hosteli 1 ya wasichana katika shule ya Sekondari Dakama unaendelea kwa ajili ya maandalizi ya kufungua kidato cha tano.
- Ukamilishaji wa nyumba 3 za walimu katika shule mpya za Sekondari za Igunda, Sabasabini na Nyankende unaendelea.

Pamoja na shughuli zillizotekelezwa, mambo yafuatayo yalifanyika:-

- Utafiti wa awali juu ya ulishaji wa watoto wa miaka miatano ngazi ya kaya umefanyika katika Mkoa wa Shinyanga kupitia Halmashauri ya Kishapu na Halmashauri ya Mji ambapo Mratibu wa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu alishiriki.

- Mafunzo maalum kwa Waratibu wa Lishe wa Halmashauri yametolewa kwa muda wa siku 10.
- Watumishi 4 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu wamepata mafunzo ya ukufunzi wa waelimishaji kuhusu ulishaji wa watoto kwa muda wa siku 5 Mkoani Shinyanga.

Kamati pia ilipitia na kujadili taarifa ya upungufu wa madawati na mikakati ya kumaliza tatizo hilo. Kamati ilikasimu majukumu ya utekelezaji wake kwa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kwa lengo la kujadili uwezekano wa kutumia misitu ya Halmashauri lakini taarifa hiyo haikujadiliwa kwenye kamati hiyo ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira badala yake ilipelekwa kwenye kamati ya Fedha, Utawala na Mipango katika kikao cha tarehe 30/04/2015.

Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kwa niaba ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji, walikubaliana yafuatayo:-

- Miti inayopatikana katika maeneo ya serikali za vijiji itumike katika kutengeneza madawati
- Zoezi hili lifanyike kwa kushirikisha kamati za shule
- Wazazi wagawane uchangiaji wa gharama za utengenezaji wa madawati, Mfano, kaya tatu zinaweza kuchangia utengenezaji wa dawati moja.
- Kamati za shule kwa kushirikiana na serilikali ya kijiji na wazazi wakarabati madawati yote yaliyoharibika
- Kila shule ipande shamba la miti ekari mbili. Hii itasaidia kutatua tatizo hili kwa kipindi kijacho. Utengenezaji wa madawati uwe umekamilika ifikapo tarehe 30/06/2015.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-
Mhe. Hamis Majogoro alisema kuwa kata ya Ubagwe ina takribani wakazi 21,000 lakini ina shule ya msingi moja tu. Alishauri kata hiyo ipewe kipaumbele mwaka 2015/2016 katika ujenzi wa shule za msingi.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema kuwa bajeti ya 2015/2016 imeshapitishwa, hivyo kama suala la ujenzi lipo kwenye bajeti, ushauri huo utazingatiwa.

D: KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO
Mhe. Tabu R. Katoto aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kwa kuzingatia taarifa za vikao na mihtasari iliyothibitishwa kwa kipindi cha robo ya tatu, Januari – Machi, 2014/2015. Vikao hivyo ni:-

- Kikao maalum cha bajeti ya 2015/2016 cha tarehe 16/01/2015 na muhtasari wake kuthibitisha tarehe 27/02/2015.
- Kikao cha kawaida cha mwezi Januari kilichofanyika tarehe 02/02/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 27/02/2015.
- Kikao cha kawaida cha mwezi Februari kilichofanyika tarehe 27/02/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 30/03/2015.
- Kikao cha kawaida cha mwezi Machi kilichofanyika tarehe 30/03/2015 na muhtasari wake kuthibitishwa tarehe 30/04/2015.

Mambo yaliyojadiliwa na Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango katika kipindi cha robo ya tatu (Januari-Machi) 2014/2015 ni pamoja na:-

- Bajeti ya Halmasharui ya Wilaya ya Ushetu kwa mwaka 2015/2016 iliyokuwa na makisio ya mapato na matumizi ya shilingi 20,485,056,914.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali iliidhinishwa.
- Kamati ilipitia na kuridhia tathmini ya zabuni Na. LGA/162/2014/2015/G/33 ya ununuzi wa mitambo ya kutengeneza barabara ambayo ni “Vibrating roller na Motor grader”. Mzabuni aliyependekezwa ni M/S Pan Africa Equipment (T) Ltd wa SLP 40575 Dar es salaam kwa jumla ya shilingi 629,820,753.00. Pia kamati iliridhia zabuni Na. LGA/162/2014/2015/W/BUILD/12 uchimbaji wa visima vinne (4) katika vijiji vya Kangeme, Iboja, Mbika na Mpunze. Mzabuni aliyependekezwa ni M/S PNR service Ltd wa SLP 6014 Dar es salaam kwa jumla ya shilingi 65,235,000.00.
- Wajumbe wa kamati ya Fedha walikubaliana kuwa hatua za kutoza ushuru katika machimbo ya Mwabomba zianze kutekelezwa ikiwa ni pamoja makampuni madogo ya uchimbaji madini kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri kama sheria zinavyoelekeza.
- Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2014/2015 ilifanyiwa marekebisho na kuwa Tshs. 2,025,000,000.00 badala ya Tshs. 2,370,000,000.00
- Kamati iliridhia marekebisho ya bajeti kwa mwaka 2014/2015 sambamba na marekebisho ya matumizi ya bajeti Tshs. 507,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya maabara za shule za sekondari.
- Kamati ilijadili shauri la nidhamu la mtumishi.
- Magulio ya Uyogo, Bugomba A, Bugomba B, Nyankende, Nyamtengera, Mbika, Igwamanoni na Kangeme hayakupata wazabuni wa kukusanya ushuru kwa kipindi cha Januari - Juni 2015. Kamati ilikubaliana kuwa kwa muda huu ambao siyo msimu wa mavuno waachwe Watendaji

wasimamie makusanyo lakini wawekewe malengo ya ukusanyaji, msimu wa mavuno utakapokuwa mzuri zabuni itangazwe.

- Kuhusu hifadhi ya msitu wa Mpunze

- Mtendaji wa Kata alindikiwa barua ili awatambue watu wote wanaolima ndani ya hifadhi hii, wakishafahamika watajulishwa/wataelimishwa kwamba hawaruhusiwi kuendesha shughuli zozote ndani ya msitu wa hifadhi.
- Watakaokaidi agizo/amri ya kuondoka, inabidi waondolewe kwa kutumia nguvu.
- Kuhakiki mipaka ya msitu wa Mpunze ili kuweka alama pamoja na mbao zinazoonesha kuwa hii ni hifadhi na hairuhusiwi kuingia au kuendesha shughuli zozote za kibinadamu ndani ya hifadhi.
- Kufanya ukaguzi ndani ya msitu wa hifadhi na kuona uharibifu uliofanyika ili kupanga jinsi ya kupunguza/kuzuia uharibifu huo na kuongeza doria za mara kwa mara.

- Kamati ya Fedha ilipitia na kujadili taarifa ya Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Desemba) 2014/2015 na ilitoa maoni yake.
- Taarifa ya kuvunjwa kwa Mkataba wa ukusanyaji wa ushuru katika machimbo ya Mwabomba ilijadiliwa. Kamati ilipata ushauri wa kitaalam kuwa katika kanuni ya 6 ya sheria ya manunuzi, kijiji kuchukua zabuni ya makusanyo siyo sawa kwani kijiji ni sehemu ya Halmashauri hivyo kijiji hakikuruhusiwa kukusanya ushuru.
- Shauri dhidi ya Ndg. Lusendamila Masanyiwa (mzabuni) anayedaiwa na Halmashauri lilifikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria.
- Kamati kwa pamoja walikubali kuupokea ufadhili wa mradi wa ujenzi wa bwawa la umwagiliaji unaotarajiwa kufadhilliwa na OX-AM GB ya Shinyanga ambapo Halmashauri itachangia shilingi 50,000,000.00 na Oxfam – GB watafadhili shilingi 50,000,000.00, na kwamba mradi huo utatekelezwa katika kijiji cha Nyamilangano.
-

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-
Mhe. Emanuel Nding'wa alitaka kujua mzabuni ndg. Lusendamila anadaiwa kiasi gani. Pia alitaka kujua kuhusu hatua inayoendelea katika kuvunjwa mkataba wa ukusanyaji wa ushuru wa machimbo.

Mhe. Sospeter Bunende alitaka kiambatisho cha ufafanuzi wa makato ya fedha za mkopo toka CRDB kwa waheshimiwa Madiwani.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema kuwa kiambatisho hakikuwekwa kwa sababu masuala ya kibenki ni ya kibinafsi, na kwamba suala la deni la benki ni siri ya mkopaji.

Kuhusu ushuru wa Mwabomba
Alieleza kuwa Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji (W) na Kamati ya Ulinzi na Usalama (W) wamepanga kwenda Mwabomba hivi karibuni.

Kuhusu deni la Lusendamila (mzabuni)
Kaimu Mweka Hazina (W) alisema kuwa Lusendamila anadaiwa shilingi 5,300,000.00 . Hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa ili wadaiwa wote waweze kulipa madeni wanayodaiwa na Halmashauri.

E: BODI YA ZABUNI
Kaimu Afisa Ugavi (W) aliwasilisha taarifa hiyo. Alisema kuwa katika kipindi cha robo ya tatu (Januari – Machi) 2014/2015 Bodi ya Zabuni ilifanya manunuzi ya shajala za ofisi, mafuta ya magari na pikipiki, manunuzi ya matairi ya magari, vifaa vya ujenzi wa maabara za shule za sekondari, matengenezo ya magari na jenereta, mikakati ya ununuzi wa mitambo ya barabara na uchimbaji wa visima virefu.

Taarifa hiyo iliyokuwa na mchanganuo wa manunuzi husika, mzabuni na thamani ya kazi/manunuzi husika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Mhe. Mohamed A. Mwarabu alisema kuwa wakaguzi walipotembelea shule ya sekondari Chona, waligundua kuwepo kwa popo wanaoharibu paa na kushauri inunuliwe dawa ili kuwadhibiti. Alitaka kujua ni lini dawa ya kudhibiti popo itanunuliwa.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa ofisi yake imepanga kununua dawa na vifaa vya kudhibiti popo katika shule zote na mchakato unaendelea.

MUHT. NA. BM/62/2014/2015 - TAARIFA YA ZIARA YA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KUTEMBELEA MIRADI YA MAENDELEO YA HALMASHAURI ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI, 2015) TAREHE 28 – 30/04/2015

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa hiyo, alisema kuwa ziara ilifanyika kwa siku 2 ambapo timu ya waheshimiwa Madiwani pamoja na wataalamu walitembelea katika Kata mbalimbali na kukagua miradi ya maendeleo katika vijiji vya Chambo, Chona, Sabasabini, Bulungwa, Ibelansuha, Kangeme, Igunda na Ilemve.
Changamoto zilizobainika kwa ujumla wakati wa tathmini ni kama zifuatazo:-

- Wanasiasa kupotosha jamii kwa kuishawishi isichangie miradi ya maendeleo mfano Kata ya Chona ambapo wanafunzi walilazimika kuchota maji kwa ajili ya ujenzi wa maabara jambo ambalo lilipaswa kufanywa na wananchi
- Baadhi ya Maafisa Watendaji wa Vijiji kutoshiriki kikamilifu kuchangisha wananchi kwa kuwa ajira zao ni za muda mfupi (hawajiamini katika kufanya maamuzi).
- Walimu waliohamishwa kwenda kwenye shule mpya za sekondari kutolipwa gharama za uhamisho.
  Hata hivyo baada ya kuwasiliana na Afisa Elimu Sekondari (W), imethibitika kuwa madai ya walimu waliohamishiwa katika shule mpya za sekondari za Igunda, Nyankende na Sabasabini yameshapokelewa na kufanyiwa uhakiki ambapo jumla ya walimu 13 walihakikiwa madai yao yenye thamani ya Tshs. 22,205,360.00 Kutokana na hali ya kifedha ya Halmashauri kutokuwa nzuri, kwa sasa malipo hayo yamesimama ila yatafanyiwa kazi pindi tu fedha zitakapopatikana

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Mhe. Moahamed A. Mwarabu alisema taarifaya kamati imetaja wanasiasa kupotosha jamii kwa kuishawishi isichangie miradi ya maendeleo mathalani Kata ya Chona, ambapo wanafunzi walilazimika kuchota maji kwa ajili ya ujenzi wa maabara jambo ambalo lilipaswa kufanywa na wananchi. Alisema kuwa suala hilo halipo kata ya chona kwani wananchi wameshiriki kikamilifu kuchangia ujenzi wa maabara na miradi mingine mingi ya maendeleo.

Mwenyekiti alieleza kuwa suala la wanasiasa kushawishi wananchi wasichangie miradi ya maendeleo linaweza kufanywa na mwanasiasa ndani au nje ya kata yake, hivyo changamoto hiyo ni ya kweli na imebainiwa na wajumbe wa kamati ya Fedha wakati wa ziara.

MUHT. NA. BM/63/2014/2015 – KUFUNGA MKUTANO

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwashukuru wajumbe na wataalam kushiriki mkutano huo. Alieleza kuwa mitambo miwili ya kutengeneza barabara imeshanunuliwa, kinachofuata ni kuajiri kwa muda madereva wa kuendesha mitambo hiyo na kununua gari la kubebea mitambo (low loader) ili kuweza kuisafirisha kwenda kwenye miradi (site). Hayo yakikamilika, utaratibu mzima wa namna ya kutumia mitambo kwa shughuli za barabara za Halmashauri na kukodisha itawasilishwa kwa wajumbe kwa majadiliano.

Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha mwenyekiti kufunga mkutano.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kushiriki mkutano huo na kusema kuwa ushauri na maagizo yaliyotolewa mkutanoni yatekelezwe. Aliwasihi waheshimiwa madiwani kufanya kazi kwa ushirikiano, kuvumiliana, kuombeana mema na kusameheana pale mmoja wao anapokosea.

Mwenyekiti alifunga mkutano saa 07:58 mchana.

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA

NA

| | | |
|---|---|---|
| ..... | ..... | ..... |
| Ndg. Isabela O. Chilumba | TAREHE | Mhe. Juma A. Kimisha |
| KATIBU | | MWENYEKITI |